## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

Namba ya simu: +255 763 320 102

Tovuti: www.fwitc.ac.tz

Barua pepe: info@fwitc.ac.tz

Chuo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu
S.L.P 516,
Mafinga-Tanzania.
Kitalu Na 12-22 nyumba H

### CHUO CHA MAFUNZO YA MISITU NA VIWANDA VYA MISITU, MAFINGA

### NAFASI ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA MISITU NA UCHAKATAJI MAZAO YA MISITU NGAZI YA VET LEVEL I - III KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026

Mkuu wa Chuo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu kilichopo Mafinga - Iringa anatangaza nafasi za maombi ya kujiunga na mafunzo kwa fani za Uhudumu misitu na Uchakataji wa mazao ya misitu ngazi ya VET Level I - III kwa mwaka wa masomo 2025/2026.

**A. Kozi zinazotolewa:**

i. Astashahada ya Uhudumu misitu ngazi ya VET Level I – III - Miaka miwili (2);

ii. Astashahada ya Uchakataji wa Mazao ya Misitu ngazi ya VET Level I – III - Miaka miwili; (2);

**B. Sifa za mwombaji:**

**i. Astashahada ya Uhudumu misitu – VET Level I - III;**

- Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu elimu ya kidato cha nne na ufaulu wa angalau alama **D** katika masomo mawili.

**ii. Astashahada ya Uchakataji wa Mazao ya Misitu – VET Level I - III;**

- Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu elimu ya kidato cha nne na ufaulu wa angalau alama **D** ya somo moja kati ya Biolojia au Kemia

**C. Jinsi ya Kutuma maombi:**

I. Mwombaji atatakiwa kujaza fomu na kuituma ikiwa na vielelezo vyote muhimu.

II. Fomu za maombi zinapatikana katika chuo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu - Mafinga na kupitia tovuti ya ***[www.fwitc.ac.tz];***

III. Maombi yote yaambatanishwe na vivuli vya vyeti halisi na taarifa za matokeo katika lugha ya Kiingereza. Endapo mwombaji atakuwa na Ufadhili, uthibitisho wa maandishi kuhusu Ufadhili huo utahitajika;

**D. Ada ya mafunzo**

Ada kwa mwaka wa kwanza itakuwa ***Sh. 940,000/=*** na inaweza kulipwa katika awamu nne, yaani kila awamu ***Sh. 235,000/=.***

**E. Fursa kwa mhitimu baada ya kumaliza masomo**

Baada ya kumaliza masomo mhitimu anaweza kujiajiri au kuajiriwa katika Mashamba ya miti ya serikali au binafsi, Taasisi za utafiti, Taasisi za mafunzo, Wakala za serikali, Serikali za mitaa, Miradi mbalimbali, Viwanda vya misitu na Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO' s)

**F. Tahadhari**

I. Kwa yeyote ambaye hatazingatia utaratibu uliotajwa hapo juu, maombi yake hayatafikiriwa. Aidha, mwombaji atakayewasilisha hati za kughushi atachukuliwa hatua za kisheria;

II. Maombi yote yatumwe kupitia anwani ifuatayo: - **Mkuu wa chuo, chuo cha Misitu na Viwanda vya misitu, S.L.P 516, Mafinga au kupitia email ya *info@fwitc.ac.tz***

III. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe ***30 Juni, 2025***

**G. Taarifa kwa watakaochaguliwa;**

Majina ya wataochaguliwa pamoja na maelezo ya kujiunga na Chuo yatawekwa kwenye tovuti ya chuo ya *(**http//www.fwitc.ac.tz**)*

**Kwa mawasiliano Zaidi +255763320102**

**Nyote mnakaribishwa**